# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

**13 MEI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 13 MEI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

### 322. MHESHIMIWA CHRISTINA SOLOMON MNDEME (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Watumishi wa Afya katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Mkoa wa Tabora.

### 323. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kuegesha Maroli Nyakahura Wilayani Biharamulo, kama alivyoelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**324. MHESHIMIWA BENJAMIN LUKUBHA NGAYIWA (KAHAMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Barabara za Mitaa na Kata za pembezoni mwa Manispaa ya Kahama.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**325. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kwa nini Serikali haipandishi hadhi NEMC kuwa Mamlaka ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**326. MHESHIMIWA JESCA JOHN MAGUFULI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uelewa kwa Vijana kuhusu athari za kujiingiza kwenye migogoro ya Kimataifa kama vile Vita ya Ukraine na Urusi.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**327. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itabadilisha Kifungu cha 13 cha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambacho kinaruhusu Mtoto wa Kike kuolewa na umri wa miaka 15.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**328. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza kuboresha Bandari ya Musoma ili Meli ya *New* MV Mwanza ianze safari za kuelekea Musoma Mjini – Kisumu hadi Jinja.

**329. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itasimamia kupunguza nauli za Mabasi na Vyombo vya Usafiri kutoka Ifakara, Mang'ula hadi Mkamba Kidatu.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**330. MHESHIMIWA TIMIDA MPOKI FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, vigezo gani vinatumika kupima ufanisi wa mageuzi ya Mitaala baada ya kusisitiza Elimu ya Amali ili kupunguza pengo la Elimu na soko la ajira kwa Vijana.

## WIZARA YA MAJI:

**331. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (MISSENYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kata ya Kashenye, Kanyizo na Bwanjai utakamilika.

**332. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, mpango wa kuyapeleka maji ya Ziwa Tanganyika katika maeneo jirani kama vile Mpanda Katavi umefikia wapi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**333. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, upi mpango wa Serikali kuwalipa fidia Wananchi wa Kitongoji cha Isela Ndolezi ili kupisha upanuzi wa eneo la Kimondo na kuleta Wanyamapori.

**WIZARA YA UJENZI:**

**334. MHESHIMIWA MOSES CHARLES BUJAGA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Ngudu – Malya (Km 24 – *Package* II) itakamilika kwa kiwango cha lami ili kuimarisha usafiri kati ya Majimbo ya Sumve na Kwimba.

**335. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (CHAMAZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mbande - Kisewe hadi Msongola utakamilika kwa kuzingatia umuhimu wake.

**336. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Nyakahanga – Benako.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA UCHUKUZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**13 MEI, 2026** **KATIBU WA BUNGE**

BUNGE LA TANZANIA
PARLIAMENT OF TANZANIA